

## **MAKUBALIANO YA MKATABA WA KUPANGA ENEO**

Makubaliano haya yamefanyika leo Tarehe 25 Decemba 2022 katika eneo la Kasamiko kata ya Sangabuye wilaya ya Ilemela na Mkoa wa Mwanza.

### **KATI YA**

Ndg **REVOCATUS PAUL MGAWE** wa SLP 1961 **MWANZA** ambaye katika mkabata huu anajulikana kama **MWENYE ENEO** neno ambalo hakuna Budi litamaanisha pia Warithi wake au watu wote wanaoweza kudai haki yoyote chini yake au kwa niaba yake kwa upande mmoja

### **NA**

M/s, **THE BIG BEST COMPANY LIMITED (GOODWARD MULUBWA)** wa **S.L.P 6252 MWANZA** ambaye katika mkataba huu anajulikana kama **MPANGAJI WA ENEO** neno ambalo hakuna Budi litamaanisha pia kwa wakurugenzi Wenza na kwa Warithi wao au watu wote wanaoweza kudai haki yoyote chini yao au kwa niaba yao au Kampuni hiyo kwa upande mmoja.

Kwa kuwa **MWENYE ENEO** ni mmiliki halali wa ENEO lililopo katika eneo la Mwaloni **Kasamiko**, katika mtaa wa Cheti kata ya Sangabuye Wilaya ya Ilemela Mkoa wa Mwanza. Eneo hilo lina ukubwa wa mita za mraba 5400.

### **BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO;**

1. Mpagaji atalazimika kumlipa Mwenye eneo kiasi cha Shilingi Laki moja (Tsh 100,000) kwa mwezi
2. Kwamba Mpagaji atatakiwa kulipa shilingi milioni tatu na laki sita (Tsh 3,600,000/=) kama kodi ya miaka mitatu ambayo ameilipa yote leo.
3. Kwamba mpangaji anaruhusiwa kufanya uwekezaji katika eneo kwa kumshirikisha Mwenye eneo na wataalamu wake.
4. Kwamba Mwenye Eneo atalazika kukatwa kidogo kidogo pesa za uwekezaji zitakazo tumiwa na Mpagaji kwa kipindi kisicho zidi miaka 20.
5. Kwamba Mpagaji atalipa pesa ya pango huku akimkata mwenye eneo kwa asilimia sabini (70%) ya gharama zote zitakazo tumika kwa kuendeleza Eneo.
6. Kwamba Mpagaji atamsamehe mwenye Eneo kiasi cha asilimia Thelasini (30%) ya gharama zote atakazo zitumia katika uwekezaji.
7. Kwamba baada ya miaka Ishirini (20) Mwenye eneo ataingia ubia na Mpagaji kwa asilimia zisizo zidi sita (6%).



8. Kwamba mpangaji atalazimika kulipa kodi zote za serikari huku akidumisha mahusiano na wenyeji wa eneo hilo.
9. Kwamba mkataba huu utakuwa kwa kipindi cha miaka miaka ishirini (20) kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba isitoshe pindi muda wa mkataba huu utakapo fikia ukomo Basi pande zote mbili zinaweza kukubaliana juu ya kuendelea au kuvunjwa kwa makubaliano haya.
10. Kwamba gharama za kuvunja mkataba zitaingiwa na atakaye amua kuvunja mkataba huu baada ya kuridhiwa na pande zote.

**KAMA USHUHUDA WA KUKUBALIANA NA VIPENGELE VYA MKATABA HUU PANDE ZOTE MBILI ZINAWEKA SAHIHI SEHEMU ZA MAJINA YAO KAMA IFUATAVYO:**

**UMESAINIWA na KUTOLEWA na**

**REVOCATUS PAUL MGAWE**

ambaye mmiliki/ msimamizi wa Enco' tajwa hapo juu

**MBELE YANGU:**

**JINA: FREDRICK KAKULWA**

SAHIHI:





**MWENYE ENEO**

**UMESAINIWA na KUTOLEWA na**

**GOODWARD MULUBWA (MKURUGENZI)**

Ambaye ni Mpangaji wa Eneo tajwa hapo juu

**MBELE YANGU:**

**JINA: FREDRICK KAKULWA**

SAHIHI:





**MPANGAJI**